TANGAZO LA SERIKALI Na. 276 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ya Mwaka 2021 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2017 ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya Tangazo la Serikali Na.29 la Mwaka 2017

2. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 4 kwa kufuta kifungu kidogo cha (5) na kuweka kipya na kuongeza kifungu kidogo cha (6) ambacho kitasomeka;

4. (5) Kikundi chochote kinachohitaji kusajiliwa ndani ya Halmashauri kitawajibika kulipa ada ya usajili ya kiasi kisichozidi shilingi 10,000/=

(6) Bila kuathiri kifungu kidogo cha 4, malipo yote yatafanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yaani I - tax au kwa mfumo wa kawaida wa stakabadhi za Halmashauri pale ambapo mfumo wa I – tax utakaposhindikana.

3. Marekebisho yanafanyika kwa kufuta kifungu cha 12.

4. Marekebisho yanafanyika kwa kufuta kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo Kuu na kuweka kifungu kipya kinachosomeka;

13. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shillingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa.

Marekebisho ya majedwali

Marekebisho yanafanyika katika Sheria Ndogo Kuu kwa kufuta Jedwali la Kwanza, Tatu, Nne, Tano, Sita, Nane, Kumi na tatu, na Ishirini na Tano na kuengeza majedwali mapya kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA
ADA YA MAJENGO NA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

| NA. | HUDUMA | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za Halmashauri<br>(a) Kubwa<br>(b) Za kati<br>(c) ndogo | <br>Tshs. 50,000/= kwa mwezi<br>Tshs. 40,000/= kwa mwezi<br>Tshs. 30,000/= kwa mwezi |
| 2 | Ukumbi mkubwa | Tshs. 50,000/= Kwa siku |
| 3 | Ukumbi mdogo | Tshs. 30,000/= kwa siku |
| 4 | viti | Tshs. 500/= kwa kila kiti kwa siku |
| 5 | Masoko yote ya Halmashauri | Tshs. 4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 6 | Mzunguko wa Stendi kuu | Tshs. 4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 7 | Maeneo Mengine ya Halmashauri | Tshs. 4,000/= kwa mita za mraba kwa mwezi |
| 8 | Pango la Chumba | Tshs. 20,000/= kwa mwezi |

JEDWALI LA SITA
ADA NA USHURU WA STEDI

| NA. | CHOMBO CHA USAFIRI/MTU | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki au baiskeli | Tshs 500/=, kuingia/kutoka kwa siku |
| 1 | Teksi au gari dogo chini ya abiria 6 | Tshs 1,000/= kutoka kwa siku |
| 2 | Basi chini ya abiria 25 | Tshs 1,500/=kutoka kwa siku |
| 3 | Basi Zaidi ya abiria 25 | Tshs 2,500/= kutoka kwa siku |
| 4 | Mtu | Tshs 200/= kuingia kwa siku |

JEDWALI LA NANE
USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NA. | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | MADNI YA UJENZI | |
| | A. MCHANGA<br>1. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>2. Tripu moja ya Power tiller<br>3. Tripu Moja ya Lori | <br>Tshs.2,000/=<br>Tshs. 2,000/=<br>Tshs. 5,500/= |
| | B. MAWE<br>4. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>5. Tripu moja ya Power tiller<br>6. Tripu Moja ya Lori | <br>Tshs. 2,000/=<br>Tshs. 2,500/=<br>Tshs. 5,500/= |
| | C. KOKOTO<br>7. Tripu moja ya mkokoteni wa Ng'ombe<br>8. Tripu moja ya Power tiller | <br>Tshs. 1,500/=<br>Tshs. 1,500/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 9. | Tripu Moja ya Lori | Tshs. 5,000/= |
| 2 | D. | MAKAA YA MAWE | |
| | 1.<br>2.<br>3. | Gari Tani 1 – 6.9<br>Gari Tani 7 – 14.9<br>Gari Tani 15 – 25 | Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 10,000/=<br>Tshs. 15,000/= |
| 3 | E. | MADINI MENGINE | |
| | 4.<br>5.<br>6. | Gari Tani 1 – 6.9<br>Gari Tani 7 – 14.9<br>Gari Tani 15 – 25 | Tshs. 5,000/=<br>Tshs. 10,000/=<br>Tshs. 15,000/= |

JEDWALI LA KUMI NA TATU

*(Limetengenezwa Chini ya kifungu cha 4)*

ADA YA MAJENGO, UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Ada ya kibali cha ujenzi na ukaguzi wa ramani | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Jengo la makazi | Tshs. 15,000/= |
| 2 | Jengo la makazi la ghorofa moja | Tshs. 30,000/= |
| 3 | Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja | Tshs. 50,000/= |
| 4 | Jengo la makazi na biashara | Tshs. 20,000/= |
| 5 | Jengo la biashara | Tshs. 25,000/= |
| 6 | Jengo la biashara zaidi ya ghorofa moja | Tshs. 70,000/= |
| 7 | Jengo la kiwanda kidogo na ghala | Tshs. 50,000/= |
| 8 | Jengo la kiwanda au kituo cha mafuta | Tshs. 150,000/= |
| 9 | Mnara | Tshs. 300,000/= |
| 10 | Jengo la taasisi ya dini, NGO, Chama cha Siasa | Tshs. 20,000/= |
| 11 | Jengo la taasisi ya dini, NGO, Chama cha Siasa | Tshs. 50,000/= |
| 12 | Kibali cha kubadili matumizi ya jingo(alteration) | Tshs. 30,000/= |
| 13 | Ukaguzi wa Ramani | Tshs. 20,000/= |
| 14 | Ada za Maombi ya Upimaji na Utumiaji wa Ardhi<br>1. Maombi ya Kiwanja au Ardhi<br>2. Ada ya malipo ya awali kwa upimaji wa kujigharamia<br>3. Ada ya malipo ya awali ya kiwanja au Ardhi (Premiun)<br>4. Ada ya upimaji na usafishaji viwanja<br>(a) Ujazo wa juu (High density)<br>(b) Ujazo wa kati (Medium density)<br>(c) Ujazo wa chini (Low Density)<br>(d) Taasisi za watu binafsi na dini<br>(e) Viwanda<br>(f) Mashamba<br>5. Kurudia upimaji baada ya mipaka kufutika<br>6. Kurudia kuonesha kiwanja baada ya | <br>Tshs. 20,000/=<br>2.5% ya thamani ya Ardhi<br><br>7.5% ya thamani ya Ardhi<br><br><br>Tshs. 40,000/=<br>Tshs. 50,000/=<br>Tshs. 60,000/=<br>Tshs. 100,000/=<br>Tshs. 100,000/=<br>Tshs. 100,000/= kwa kila ekari<br>50% ya ada ya upimaji<br>Tshs. 10,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | ugavi wa awali kufanyiaka<br>7. Ukaguzi wa nyaraka<br>8. Ada ya kuomba nakara ya nyaraka | Tshs. 20,000/=<br>Tshs. 10,000/= |

JEDWALI LA ISHIRINI NA TANO
USHURU WA BIDHAA ZITOKANAZO NA MAZAO

| NA. | BIDHAA | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Pumba | Tshs Tshs 1,000/= Kwa Gunia |
| 2 | Mashudu | Tshs 1,000/= Kwa Gunia |
| 3 | Bidhaa Nyingine | Tshs 1,000/= Kwa Gunia |

Mabadiriko haya yanasomeka pamoja na Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi iliyobandikwa kwenye Marekebisho ya Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ya mwaka 2019 kufuatia azimio lililopitishwa na mkutano wa halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 28/2/2020. Na Nembo hii inabandikwa:-

MISSANA K KWANGURA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

SUMUNI ZENO MWANAKULYA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
3 Machi, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*